## MUHTASARI WA MAHITAJI MAHSUSI YA BAJETI KWA AJILI YA VIPAUMBELE VYA SEKTA YA ELIMU KWA MWAKA 2026/27 HADI 2029/30

### 1. UTANGULIZI

Sekta ya Elimu katika mwaka 2026/27 imeandaa vipaumbele vya kisekta vilivyotokana na maboresho ya Sera ya Elimu 2014, Toleo la 2023 na hotuba ya Mhe Rais wakati wa ufunguzi wa Bunge la 13 mnamo tarehe 14 Novemba, 2025.

Mapendekezo ya vipaumbele vya kisekta ni mahsusi na yamebainishwa kwa kuzingatia **mahitaji mapya na mahitaji ya lazima** kwa miaka minne kuanzia 2026/27 hadi 2029/30 na pia yameonesha mahitaji kwa mwaka mmoja wa fedha wa 2026/27 **(rejea kiambatisho cha gharama za kisekta)**. **Aidha, kwa kuwa gharama hizi ni mahsusi hazijajumuisha mahitaji ya mishahara, uendeshaji na baadhi ya miradi ya maendeleo zitapelekea kuongeza tengeo la bajeti ya kisekta kwa mwaka 2026/27.**

Baadhi ya vipaumbele vya kisekta ni kama ifuatavyo na vimejitokeza kwa ujumla wake katika kiambata kinachoonesha gharama za vipaumbele vya kisekta:

i. Maandalizi ya Makundi Rika Mawili (Double Cohort);
ii. Uendeshaji wa Bodi ya Walimu Tanzania (TTPB);
iii. Kuanzisha Maabara za Kitaifa za Rufaa katika Utafiti na Ubunifu wa Viwanda (National Reference Industrial Research and Innovation Laboratories);
iv. Kuanzisha vituo saba (7) vya kitaifa vya ubunifu, uendelezaji na ubiasharishaji wa bunifu na teknolojia zinazoibuliwa nchini katika maeneo ya kimkakati (Specialized National Innovation, Commercialization and Entrepreneurship (SNICE) Hubs;
v. Ufadhili kupitia Samia Extended Schorlaship DS/AI+ na Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati;
vi. Ununuzi wa Vifaa vya shule za amali;
vii. Mazoezi ya Walimu kwa Vitendo (Internship);
viii. Vituo vipya vya ubainishaji na upimaji wa kielimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
ix. Kukamilisha shule maalum za Sekondari za Wasichana na Wavulana za Sayansi katika kila Mkoa;

x. Ujenzi wa VETA 65 na ununuzi wa vifaa katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;
xi. Kuunganisha kwa njia ya kidijitali shule za vijijini na mijini ili kubadilishana uzoefu na taarifa;
xii. Shule ya kusomea nyumbani kwa ajili ya wanafunzi wenye changamoto ya afya na kiwango cha juu cha ulemavu;na
xiii. Ununuzi wa vitabu vya ziada katika shule za sekondari za kidato cha Tano na Sita.

Kwa kuzingatia masuala mbalimbali ya utengaji wa bajeti, ufuatao ni muhtasari unaonesha mchanganuo wa mahitaji na gharama za vipaumbele vya Sekta ya Elimu kwa mwaka wa fedha 2026/27 hadi 2029/30 na mahitaji mahususi kwa mwaka wa fedha 2026/27.

**JEDWALI NA 1: MCHANGANUO WA GHARAMA ZA KISEKTA KWA KUZINGATIA MAHITAJI MAHSUSI MAPYA NA YA LAZIMA KWA MWAKA 2026/27 HADI 2029/30**

| Na | MAHITAJI YA BAJETI KWA MWAKA 2026/27 HADI 2029/30 (MIAKA MINNE) | MAHITAJI YA BAJETI YA KWA MWAKA 2026/27 (MWAKA MMOJA) |
|---|---|---|
| 1. | 35,460,455,375,715.00 | 6,914,214,765,630.63 |

## 2. UTENGAJI WA BAJETI MAHSUSI YA VIPAUMBELE VYA KISEKTA

Maeneo mahsusi ya bajeti ya kisekta yamegawanyika katika sehemu mbili ambayo ni mahitaji mpya na ya lazima kama ifuatavyo;

### a) Mahitaji Mapya

1. Maandalizi ya mapokezi ya Makundi-Rika Mawili (Double Cohort) kwa mwaka 2028. Eneo hili litahusiha ujenzi wa miundombinu ikiwemo karakana, maabara, madarasa na matundu ya vyoo, ajira za walimu na wakufunzi wa karakana pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia**;**
2. Uendeshaji wa bodi ya walimu Tanzania ambao utahusisha mishahara ya watumishi, ununuzi wa vifaa vya kieletronic na Gharama za uendeshaji (Kuandaa vyeti vya usajili na leseni, kusajili walimu, usimamizi wa interns, miongozo ya uendeshaji na kuendesha vikao na wadau)**;**
3. Ununuzi wavifaa vya amali;

4. Mazoezi ya Walimu kwa Vitendo (Internship) ambapo gharama za posho kwa walimu hao ni sh 300,000 kwa mwezi na inatarajiwa kuanza na wanafunzi 3,459 wa diploma**;**
5. Kukamilisha uanzishwaji wa madawati ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu katika Halmashauri;
6. Kuanzisha vituo vipya vya ubainishaji na upimaji wa kielimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu
7. Uanzishwaji wa Maabara za Kitaifa za Rufaa katika Utafiti na Ubunifu wa Viwanda (National Reference Industrial Research and Innovation Laboratories); na
8. Kuanzisha vituo saba (7) vya kitaifa vya ubunifu, uendelezaji na ubiasharishaji wa bunifu na teknolojia zinazoibuliwa nchini katika maeneo ya kimkakati (Specialized National Innovation, Commercialization and Entrepreneurship (SNICE) Hubs.

**b) MAHITAJI YA LAZIMA**

i. Mikopo Kwa wanafunzi Elimu ya kati na Juu kwa ajili ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wanaoendelea kwa Local Undergraduates 325,450, Local Postgraduates (Law School, Masters and PHDs) 190, Diploma 27,200, Overseas 5 na Samia Schorlaship (STEM) 3,475;

ii. Samia Extended Schorlaship DS/AI;

iii. Kukamilisha shule maalum za Sekondari za Wasichana 26 na Wavulana 7 za Sayansi katika kila Mkoa;

iv. Ujenzi wa VETA 65 (awamu ya II) na VETA 29;

v. Posho kwa watumishi mwega,stahili za walimu na chakula kwa wanafunzi wa bweni;

vi. Ununuzi wa vitabu vya kiada kwa kidato cha tano na sita;

vii. Gharama za mitihani kwa vitendo kwa vyuo vya ualimu;

viii. Dharura ya majanga shuleni;

ix. Kusimika mifumo ya nishati safi katika shule za sekondari za bweni; na

x. Kuendeleza jitihada za kuweka miundombinu na vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

## 3. HITIMISHO

Pendekezo la tengeo la bajeti mahsusi kwa kuzingatia mahitaji mapya na ya lazima kwa mwaka wa fedha 2026/27 inakadiriwa kuwa **Shilingi 6,914,214,765,630.63** ambapo **Shilingi 1,605,262,033,594.33** itatumika na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wakati **Shilingi 5,308,952,732,036.30** itatumika na OWM-TAMISEMI. ***Aidha, kiasi hiki ni mahsusi hakijajumuisha mahitaji yote ya bajeti yatakayohitajika katika bajeti ya sekta ya elimu kwa mwaka 2026/27 ikiwemo mishahara, uendeshaji na baadhi ya miradi ya maendeleo. Kwa muktadha huo bajeti ya sekta ya elimu ya mwaka 2026/27 inakadiriwa itazidi bajeti ya sekta ya elimu ya mwaka 2025/26 ambayo ni Shilingi Trilioni 7.5***